

## Chanjo za COVID-19

### Maswali Yanayoulizwa Sana kwa Wazazi, Walezi, na Vijana Wenye Umri wa Miaka 12-17 Wanaostahiki Chanjo ya Pfizer

**Je, kuna chanjo zinazotolewa kwa watoto au vijana?**

**A:** Ndiyo. Nchini Marekani, chanjo moja ya COVID-19 imeidhinishwa na Shirika la Kudhibiti Chakula na Dawa la Marekani (FDA) kwa watu wenye umri wa miaka 12 na zaidi– chanjo ya Pfizer. Chanjo ya Pfizer ilikuwa na mojawapo ya majaribio makubwa zaidi ya kimatibabu katika historia, na zaidi ya washiriki 43,000 wa hiari. Chanjo zingine zilizopo, Moderna na Johnson & Johnson, kwa sasa zimeidhinishwa kwa watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi.

**Q: Je, mzazi/mlezi anahitaji kutoa idhini?**

**A:** Ndiyo. Watoto wa chini ya umri wa miaka 18 ambao wako chini ya ulezi wa mzazi au mlezi halali sharti wawe na idhini ya mzazi au mlezi halali ili kupokea chanjo yoyote. Mzazi au mlezi halali anapaswa kuandamana na mtoto anapoenda kupokea chanjo, isipokuwa kama chanjo hiyo inatolewa ofisini mwa daktari, shuleni au kliniki ya shule au mazingira kama hayo.

**Q: Je, chanjo zote za COVID-19 ni salama na zenye ufanisi?**

**A:** Ndiyo, chanjo za COVID-19 ni salama na zina ufanisi. Kulingana na FDA, katika [jaribio la kimatibabu la chanjo](#) ya Pfizer kwa vijana wenye umri wa miaka 12-15, hakuna mtoto kati ya watoto 1,100 waliopokea chanjo ya Pfizer aliyeambukizwa COVID-19, na watoto 16 kati ya 1,100 waliopokea kipozauongo. Jaribio hilo pia liligundua kuwa vijana waliopokea chanjo walikwa na viwango vya juu vya kingamwili kwenye damu yao, kuonyesha kwamba walikuwa wamesitawisha kinga dhabiti.

**Q: Chanjo inachukua muda gani kufanya kazi?**

**A:** Chanjo ya Pfizer inatolewa kwa dozi mbili. Dozi ya pili inatolewa siku 21 (wiki tatu) baada ya kupokea dozi ya kwanza. Unahitaji dozi zote mbili ili upate kinga kamili. Mtu huchukuliwa kwamba amepokea chanjo kikamilifu wiki mbili baada ya dozi ya pili.

**Q: Kupokea chanjo za COVID-19 kuna athari gani?**

**A:** Athari zinazotokea mara nyingi ni maumivu, wekundu, au kufura kwenye eneo lililodungwa sindano; homa na/au kuhisi kijibaridi; kuumwa na kichwa; uchovu; na maumivu ya misuli na maungo. Athari hizi ni za kawaida na ni ishara kwamba mwili wako unapata kinga ya kukulinda dhidi ya COVID-19. Kwa kawaida athari hizi hushuhudiwa kwa siku chache tu, na huenda zikaongezeka baada ya kupokea dozi ya pili.

**Q: Je, chanjo za COVID-19 zitabadilisha DNA ya mtu?**

**A:** Hapana. [Chanjo za COVID-19](#) hazibadilishi DNA ya mtu. Chanjo ya Pfizer ni Chanjo ya messenger RNA (mRNA). Inatoa maagizo kwa mwili kutengeneza protini ya utando inayopatikana kwenye virusi vinavyosababisha COVID-19; kisha mwili hujibu kwa kujenga kingamwili za kuharibu protini hiyo.

**Q: Je, chanjo za COVID-19 zinawapandikiza watu mwilini kidude kinachotumiwa kuwafuatilia watu?**

**A:** Hapana, sindano za chanjo hazina vidude vinavyotumiwa kuwafuatilia watu.

**Q: Chanjo za COVID-19 husababisha utasa, au kuathiri uwezo wa mtoto wa kuzaa baadaye?**

**A:** Hapana. Kwa sasa hakuna ushahidi kwamba chanjo zozote, ikijumuisha chanjo za COVID-19, husababisha shida za uzazi.

**Q: Ninawezaje kuweka miadi ya chanjo? Vijana wanaweza kupokea chanjo wapi?**

**A:** Kuna mamia ya maeneo ambayo vijana wanaweza kupokea chanjo kote jimboni, ikijumuisha ofisi za madaktari, kliniki za chanjo, idara za afya za mitaa, hospitali, vituo vya afya vya jamii, na mengine. Hata hivyo, wazazi wa watoto wenye umri wa miaka 12 wanashauriwa kwamba kwa sababu ya sheria ya jimbo ya sasa, watoto walio chini ya miaka 12 lazima wawe na agizo la daktari ili wapokee chanjo kwenye maduka ya dawa; wanaweza kupokea chanjo pahali popote isipokuwa kwenye maduka ya dawa. Vijana wenye zaidi ya miaka 13 hawahitaji agizo la daktari, na wanaweza kupokea chanjo zao za COVID-19 kwenye maduka ya dawa au kwenye maeneo mengine yanayotoa chanjo yaliyoorodheshwa katika [gettheshot.coronavirus.ohio.gov](#). Sheria ya kuwaruhusu vijana

wenye umri wa miaka 7-12 kupokea chanjo ya COVID-19 au chanjo ya homa ya mafua kwenye maduka ya dawa bila agizo la daktari inasubiri kupitishwa. Bado maagizo ya daktari yatahijika kwa chanjo zingine zote zinazotolewa kwa watu wa kikundi hiki. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Ohio na Seneti ya Ohio wamepitisha mswada huo. Mara tu mswada huo ukiwekwa saina na gavana, utaanza kutumika mara moja.

**Q: Mtoto wangu anafaa kufanya nini kabla ya miadi yake ya kupokea chanjo?**

**A:** Anafaa kula na kunywa maji mengi kabla ya kupokea chanjo. Hii ni muhimu hasa kwa watoto na vijana kwa sababu [kuzirai baada ya kupokea chanjo yoyote hutokea mara nyingi kwa vijana, na mara nyingi hutokana na wasiwasi mwingi au kuishiwa na maji mwilini](#). Ikiwezekana, pata mapumziko ya kutosha usiku kabla ya miadi yako. Vaa shati lenye mikono mifupi au lisilo na mikono ili sehemu ya juu ya mkono ifikiwe kwa urahisi. Ikiwa ni siku baridi, vaa fulana au jaketi ambalo ni rahisi kuvua haraka.

**Q: Nifanye nini ikiwa mtoto wangu ana wasiwasi?**

**A:** Mwambie mtoto wako apumue polepole na avute pumzi nyingi kabla ya kudungwa sindano na afikirie kuhusu jambo linalomtuliza. Asiangalie sirinji, na alegeze sehemu ya mkono ambapo atadungwa sindano. Wazazi wanaweza kuchukua [hatua rahisi zitakazosaidia kutayarisha wana wao kwa chanjo na kupunguza hofu](#). Wazazi wanaweza kutuliza wasiwasi wa wanao kwa kuwakumbusha kuvuta pumzi nyingi au kuwashughulisha kwa kuzungumza nao wakati wanapokea chanjo.

**Q: Nimeona uvumi mwingi kwenye mitandao ya kijamii kuhusu chanjo. Nitajuaje ukweli ni upi?**

**A:** Habari za uongo kuhusu chanjo za COVID-19 zimejaa mtandaoni, na huenda ikawa vigumu kujua cha kuamini. Unachoweza kufanya ni kujielimisha kuhusu chanjo kwa kutumia habari kutoka kwa vyanzo vinavyoaminika. Jifunze zaidi kuhusu [kupata habari zinazoaminika kuhusu chanjo kwenye makala haya ya CDC](#), na ujue tofauti ya uongo na ukweli [kwenye ukurasa huu kutoka kwa Idara ya Afya ya Ohio](#).

**Je, una maswali zaidi kuhusu COVID-19?**

[Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara](#) | [Uongo dhidi ya Ukweli](#) | [Mambo unayofaa kufahamu kabla, wakati wa kupokea chanjo ya COVID-19 na baada yake](#)

*Ilisasishwa mnamo Mei 12, 2021.*